MKUTANO MAAFISA MAGEREZA 24.10.2024 - DODOMA

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kukutana kwa ajili ya Mkutano wa Mwaka wa Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Magereza. Namshukuru pia Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kunipatia heshima ya kuja kufungua Mkutano huu unaolenga kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Magereza na kuweka mikakati ya kuboresha utendaji kazi. Nimefurahi sana kufika hapa Makao Makuu ya Jeshi la Magereza, kwa mara ya kwanza. Nawashukuru na kuwapongeza kwa jitihada zinazoziona hapa za kutunza na kupendezesha mazingira kwa miti na maua mazuri. *Landscaping* iliyofanyika hapa ni ya kiwango. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Waziri wa Ndani pamoja na Kamishna Jenerali wa Magereza na wote waliohusika kuandaa vizuri Mkutano huu.

Wahe. Viongozi na Washiriki,

Kama inavyofahamika, Jeshi la Magereza lina majukumu ya msingi ya kusimamia vifungo vya wahalifu waliohukumiwa, kuhifadhi mahabusu wakati wakisubiri hukumu, na urekebu. Kwa kutekeleza majukumu hayo, Jeshi la Magereza linaimarisha usalama wa raia kwa kuwasaidia wafungwa kujirekebisha na kurejea kuwa raia wema baada ya muda wa vifungo vyao kwisha. Hata hivyo, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (Machi 2024), kuhusu Ukaguzi wa Utekelezaji wa Programu za Urekebu, inaonesha kuwepo kwa ongezeko la wastani wa 1.5% kwa mwaka la wafungwa waliomaliza vifungo (kati ya 2019/2020 na 2022/2023) kufanya tena uhalifu na kurudi magerezani. Hii ni sawa na wafungwa 3,239 (2019), 3,384 (2020), 3,235 (2021), 4,013 (2022) na 3,262 (2023). Aidha, kwa mujibu wa utafiti uliochapishwa kwenye Jarida la Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini la mwaka 2023, wahalifu wanaoweza kurudia kufanya uhalifu baada ya kumaliza vifungo vyao ni wale wenye elimu ndogo, wasiokuwa na ajira, waliofungwa kwa makosa madogo, na wale waliokosa huduma za urekebu.

Aidha, Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali inazitaja sababu nyingi zinazopelekea wafungwa wanaomaliza vifungo vyao kufungwa tena kuwa ni pamoja na kukosekana kwa miongozo rasmi ya magereza ya namna ya kutekeleza programu za urekebu; kutokuwepo na utaratibu mzuri wa kubaini na kuwatenga wafungwa kwa ajili ya programu za urekebu kulingana na vipaji vyao; kukosekana kwa miundombinu ya kutosha inayowezesha utekelezaji wa huduma za urekebu; kutokuwepo kwa programu za kutosha za huduma za kielimu na kisaikolojia kwa wafungwa ili kuwezesha urekebu; baadhi ya Maafisa wa Magereza kukosa elimu na mbinu za urekebu kwa wafungwa; kutokuwepo na mfumo wa motisha kwa wafungwa wanaofanya vizuri kwenye programu za urekebu magerezani; kukosekana kwa ukaguzi wa utekelezaji wa huduma za urekebu; kukosekana kwa programu za kuwaandaa wafungwa wanaokaribia kumaliza vifungo; na kukosekana kwa viashiria vya upimaji wa utekelezaji wa huduma za urekebu magerezani. Hivyo, naisisitiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Magereza kuongeza kasi kufanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika taarifa ya CAG ili kuboresha huduma za urekebu. Vilevile, Jeshi la Magereza lishirikiane na Jeshi la Polisi pamoja na Bodi ya Parole kuweka utaratibu wa kuwatambua na kuwafuatilia wale wanaotoka Magerezani kwa msamaha na hata wale waliomaliza vifungo vyao wanakokwenda na jinsi wanavyoenenda.

Wahe. Viongozi na Washiriki,

Mwaka 2023 Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliunda Tume, kwa lengo la kufanya tathmini ya Mfumo wa Haki Jinai nchini na kufanya

mabadiliko ya kisheria na kimuundo ili kuboresha huduma za Haki Jinai nchini. Tume hiyo ilitoa mapendekezo: **Kwanza** kuhusu Taswira ya Jeshi la Magereza ambapo ilibaini kuwa Jeshi linatumia nguvu kupita kiasi ikiwa ni pamoja na ukaguzi unaotweza utu na kukiuka haki za binadamu; uwepo kwa msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu magerezani; uchakavu wa miundombinu; na baadhi ya wahalifu wanaomaliza kutumikia vifungo vyao kutobadilika. **Pili**, ilihusu huduma za Jeshi la Magereza ambapo ilionekana kuwa huduma zinazotolewa kwa wafungwa na mahabusu zina ufanisi mdogo. Huduma hizo ni pamoja na za kiafya, ubora wa chakula, huduma za kisheria na kiroho, na ukaguzi usio wa staha. Vilevile, watoto waliowekwa mahabusu kuchanganywa na watu wazima; kutokuwepo kwa miundombinu rafiki kwa wenye mahitaji maalum; kutokuwepo kwa magereza katika baadhi ya wilaya ambazo kuna Mahakama na vituo vya Polisi na kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika na salama wa kuwapeleka mahabusu na wafungwa mahakamani. Aidha, Tume ilibaini matumizi makubwa ya kuni kama nishati ya kupikia kunakosababisha uharibifu wa mazingira na wafungwa kutumia muda mwingi kutafuta kuni na ni miongoni mwa mambo yanayolalamikiwa na kupelekea jamii yetu kuliona Jeshi la Magereza halijali utu wa wafungwa na mahabusu, pamoja na kuchelewesha upatikanaji wa haki zao. Na hapa napenda kunukuu maneno ya Hayati Rais Nelson Mandela, wa Afrika Kusini, aliyesema, nanukuu; "*It is said that no one truly knows a nation until one has been inside its jails. A nation should not be judged by how it treats its highest citizens, but its lowest ones.*" (Kwa Kiswahili: Hakuna anayeweza kulifahamu Taifa vizuri hadi pale atakapokuwa ameingia kwenye jela zake. Taifa halipimwi kwa namna linavyowajali raia wake wenye hali ya juu bali wale wa hali ya chini). Nimefurahi kusikia kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Magereza mmeanza kufanyia kazi mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai. Ninawahimiza kuyapokea mapendekezo hayo kwa dhati na kuongeza kasi ya utekelezaji wake. Aidha, napenda kutumia fursa hii kusisitiza masuala yafuatayo:

Jambo la Kwanza; pamoja na mchakato wa Marekebisho ya Sheria ya Magereza ambao Kamishna Jenerali ameeleza kuwa unaendelea, napenda kusisitiza kuwa marekebisho hayo hayatakuwa na maana, endapo Viongozi na Maafisa Magereza hawatabadili mtazamo ili kuendana na mazingira ya sasa, kwa kuwa sheria na mfumo wa Magereza tulionao tumeurithi kutoka kwa wakoloni. Naielekeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhakikisha mchakato wa marekebisho ya Sheria unakamilika mapema na unazingatia mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai na hali ya sasa. Pamoja na mahitaji ya rasilimali zinazohitajika katika kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai kuhusu Jeshi la Magereza, mabadiliko ya mitazamo ni muhimu sana. Matumaini ya Amiri Jeshi Mkuu ni kuwa Mkutano huu usaidie kuleta mitazamo chanya ndani ya Jeshi la Magereza kuhusu mabadiliko (*reforms*). Taarifa zilizopo zinaonesha kuwa Jeshi la Magereza la Uganda ni miongoni wa majeshi yenye huduma bora za urekebu barani Afrika, licha ya changamoto ya rasilimali fedha. Hivyo, kinachohitajika zaidi ni dhamiri ya dhati na ubunifu ili kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za urekebu, na kupunguza idadi ya wanaomaliza vifungo vyao na kurejea tena magerezani. Ninapongeza mpango wa Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Ufundi, Chuo Kikuu Huria, Chuo cha Ustawi wa Jamii, VETA na NACTVET wa kuandaa mitaala mipya ya mafunzo inayoendana na wakati wa sasa. Ninashauri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Magereza kuchukua hatua zinazowezekana kwa kutumia rasiliamli zilizopo, kuondoa dhana ya kudhalilisha utu na kukiuka haki za binadamu. Hii ni pamoja na kupunguza na hatimaye kuondokana kabisa na matumizi ya ndoo magerezani kama choo. Aidha, kwa kushirikiana na wadau

mbalimbali, fanyeni juhudi kuwapatia wafungwa vifaa vitakavyowasaidia kujiendeleza kielimu wanapokuwa magerezani kama kompyuta, vitabu na vifaa vingine. Aidha, ninaamini kuwa Jeshi la Magereza linaweza kuboresha lishe ya wafungwa kwa rasilimali zilizopo na kuwapatia wafungwa wengi zaidi ujuzi wa kilimo chenye tija. Pia, inawezekana kuwawezesha wafungwa wa kike kupatiwa mafunzo mbalimbali ya kuendesha biashara, kama ile ya *saloon.* Hali kadhalika, ninalitaka Jeshi la Magereza kuweka nguvu kuimarisha michezo ili tuwe na timu nyingi bora za michezo kwa wanawake na wanaume.

Jambo la Pili, ni kuhusu Jeshi la Magereza kujitosheleza kwa chakula na kuimarisha usimamizi wa miradi inayoendeshwa na Jeshi hili. Pamoja na shughuli zinazoendelea kwa upande wa kilimo cha mazao, ufugaji na viwanda, Jeshi la Magereza bado lina nafasi kubwa ya kuongeza uzalishaji na tija katika maeneo hayo. Hivyo, Waziri wa Mambo ya Ndani ashirikiane na Wizara na Idara husika za Serikali kuwezesha ujenzi wa skimu za umwagiliaji hususan katika Magereza yenye maeneo makubwa ya kilimo nchini kama Kitete (Rukwa), Kalilankulukulu (Katavi), Pawaga (Iringa) na Ilagala (Kigoma) n.k. Hatua hii iende sambamba na kuweka utaratibu wa ununuzi au ukopaji wa zana za kilimo kutoka SUMA JKT au Kampuni nyingine binafsi zinazouza zana za kilimo. Magereza pia, iweke nguvu katika kuzalisha miche na mbegu hususan za mazao ya kimkakati ili kulisaidia Taifa kuondokana na utegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi. Hivyo hivyo, Jeshi la Magereza liimarishe uendeshaji wa viwanda vyake au vinavyoendeshwa kwa ubia, kwa ajili ya soko la ndani na hata masoko katika nchi jirani. Jeshi la Magereza pia, lifanye tathmini ya utendaji wa Magereza Corporation Sole ili kuona kama unaendana na azma ya kuanzishwa kwake. Hakikisheni kuwa mauzo na matumizi yote yanafanyika kupitia Namba rasmi ya malipo *(control number)* na risiti halali za Serikali zitolewe ili kudhibiti na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato. Pia, ninalitaka Jeshi la Magereza lijizatiti katika sekta ya ufugaji wa mifugo ya aina mbalimbali kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, samaki/viumbe maji, nyuki na ndege wa aina mbalimbali kwa ajili ya matumizi magerezani na kuuza ziada katika soko la ndani na nje ya nchi. Miradi hii ikisimamiwa vizuri, hakika inaweza kuongeza mapato ya ndani ya Jeshi la Magereza na kupunguza utegemezi kwenye bajeti ya Serikali.

Tatu; ni uhifadhi na utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi ya kupikia. Jeshi la Magereza lina nguvukazi ya kutosha kupanda na kutunza miti katika maeneo yake na maeneo mengine ikiwa ni sehemu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira nchini. Hata hivyo, maeneo mengi ya Jeshi la Magereza bado hayana miti ya kutosha na ushiriki wa Magereza katika upandaji miti katika maeneo mengine bado hautoshi. Korea Kusini ni mfano mzuri wa nchi iliyotumia Magereza kukijanisha vilima vyote katika nchi yao. Nayataka Magereza yote kuwa kielelezo cha upandaji miti ya kivuli, matunda na maua katika maeneo yake. Magereza yaliyo kando ya barabara kuu, kama ilivyo hapa Makao Makuu ya Magereza wahakikishe wanapanda miti pembezoni mwa hifadhi ya barabara, kama walivyofanya jirani zenu JKT Makutupora. Hivyo, nawataka nanyi kuendeleza kuanzia mwanzo wa *ring road* na kuelekea katikati ya Jiji la Dodoma. Vilevile, natarajia kila gereza kutunza msitu wa asili ulio karibu au kuanzisha msitu wa kielelezo kwa kupanda miti, kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo hayo na nawataka uongozi wa wilaya/mkoa wasaidie kufanikisha kazi hiyo. Aidha, pamoja na kuanza kutumia nishati safi ya kupikia kwa baadhi ya magereza, bado matumizi ya nishati ya kuni ni makubwa na hivyo kuchangia katika uharibifu wa mazingira. Kwa ajili hiyo, natoa wito kwa Jeshi la Magereza kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya nishati safi ya kupikia. Aidha, Jeshi lione namna ya kuwezesha magereza yote yanayofuga ng'ombe, kuzalisha na kutumia *biogas* kwa ajili kupikia.

Nne, na mwisho; ni matumizi ya mifumo ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na kamera za CCTV, matumizi ya Mahakama Mtandao, vifaa vya upekuzi (*walk through scanners*), na kuweka mfumo wa taarifa za wahalifu kwa ajili ya usalama wa askari, mahabusu, wafungwa na jamii kwa ujumla. Nawapongeza kwa hatua ya awali ya kufunga kamera za CCTV katika magereza 10 nchini, na kutenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya upekuzi na ujenzi wa mfumo wa taarifa za wafungwa. Nawapongeza pia kwa kuwezesha matumizi ya mahakama mtandao katika magereza 66 nchini. Vilevile, ni muhimu kuhakikisha mifumo hiyo inasomana na mifumo ya vyombo vingine vya haki jinai ili kurahisisha utendaji kazi. Hali kadhalika ninamtaka Waziri wa Mambo ya Ndani kuanza mchakato wa kujenga kwa awamu Magereza ya kisasa na ya mfano, kama ambavyo Jeshi la Polisi linavyotekeleza ujenzi wa Vituo vya Polisi vya kisasa. Kwa bahati nzuri Jeshi la Magereza lina wataalamu wa ujenzi, mafundi na nguvukazi ya kutosha.

Ninapohitimisha, ninamtaka Waziri wa Mambo ya Ndani na Uongozi wa Jeshi la Magereza kusimamia maslahi ya Askari kwa kuboresha stahili zao ikiwemo posho mbalimbali, mafunzo, vitendea kazi, upandishaji vyeo kwa haki na kuboresha makazi. Ninawaahidi kuwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake wataendelea kuliwezesha zaidi Jeshi la Magereza katika utekelezaji wa maboresho na majukumu yake.

Baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima kutamka kuwa Mkutano wa Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Magereza mwaka 2024, umefunguliwa rasmi. Nawatakia mkutano mwema.

Asanteni sana.